JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA UKIUKAJI WA AGIZO LA SERIKALI KUHUSU KUTOSOMA HABARI ZA MAGAZETINI KWA UNDANI**

**SHAURI NA. 2- 2019/20**

**TBC FM RADIO**

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA AGIZO LA SERIKALI LA KUTOSOMA HABARI ZA MAGAZETINI KWA UNDANI**

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Kituo cha Utangazaji cha TBC FM Radio cha Dar es Salaam kinatuhumiwa kukiuka Agizo la Serikali lililotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (MB), tarehe 03 Mei, 2017 kwa watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma kwa undani maudhui yaliyomo katika magazeti badala yake wasome vichwa vya habari pekee. Kimsingi, agizo hilo la Serikali lililenga kulinda soko la biashara ya uchapishaji, usambazaji, na uuzaji wa magazeti nchini.

1.2 Aidha, tarehe 15 Juni, 2017, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliviandikia barua vituo vyote vya utangazaji (ikiwa ni pamoja na kituo cha TBC FM Radio) na kuvitaka kuacha mara moja kusoma kwa undani habari za magazetini na badala yake wasome tu vichwa vya habari kwa mujibu wa agizo hilo la Serikali.

1.3 Kituo cha TBC FM Radio kinatuhumiwa kukiuka agizo hilo la serikali kupitia kipindi chake cha "**Busati**" kwenye kipengele cha "**Magazeti**" ambacho kilirushwa tarehe 02 Agosti, 2019 kati ya saa 12.00 asubuhi na saa 04.00 asubuhi. Katika kipindi hicho, mtangazaji wa kipindi alisoma kwa undani habari mbali mbali zilizoandikwa katika magazeti ya Uhuru na Habari Leo kinyume na agizo lililotolewa na Serikali.

1.4 Kitendo hicho cha kusoma taarifa hizo za magazeti kwa undani ni kupuuza kwa makusudi agizo la Serikali ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Waziri tarehe 03 Mei, 2017 jijini Mwanza wakati wa kilele cha maadhimisho ya 26 ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari duniani.

1.5 Mtangazaji wa kipindi cha Busati alikiuka agizo hilo la Serikali kwa kusoma habari za magazetini kwa undani kama ifuatavyo;

**Tarehe 02 Agosti, 2019**

**Gazeti la Uhuru Uk.2** *"Jaji Mkuu aibua hoja tano nzito, Jaji Mkuu Profesa Ibrahimu Juma ameibua hoja nzito nne za kupunguza msongamano gerezani kwa wafungwa na mahabusu ambazo pamoja na nyingine ametaka kuwapa kasi ya upelelezi wa kesi zinazoendelea mahakamani, kuna hoja tano utaangalia mwenyewe baadae lakini mi nakupa angalau dondoo tu".*

*"Hapa kuna habari picha iko Uk. 2, kiongozi wa mbio za mwenge wa Uhuru, Mzee Mkongea Ally akiweka jiwe la msingi la Ujenzi wa jengo la utawala la hospitali ya wilaya ya Ilala Kivule Dar es salaam jana picha nzuri imepigwa na Christopher Lisa".*

*"Utafutwe ufumbuzi wa kudumu kukomesha mimba za wanafunzi."*

***Maoni ya Mtangazaji**: "mimba za wanafunzi ni mafataki tu kuacha mambo hayo, we mwanafunzi akipita unamwita unamwitia nini mtu anakwenda shule anaenda shule, na wengine hao akiwapa mtu lifti ndo basi tena ndo kumekucha."*

***Mtangazaji akaendelea kusoma**: "Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Harrison Mwakyembe, mwanzoni mwa wiki hii akiwa katika ziara ya kikazi katika jimbo lake la Kyela alishtushwa na wimbi kubwa la wanafunzi wa kike wilayani Kyela kupata mimba wakiwa shuleni.*

***Maoni ya Mtangazaji**: "hawa wanaowapa waadhibiwe adhabu kali sana hao, kali kabisa, bila shaka jitihada zitaendelezwa za kupambana na hiyo hali. Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema atazidi kutuwezesha kutupa subira na kuwapa huruma hao wanaovamia mamia ya wanafunzi huko mtaani".*

*"Kilio cha askari magereza kununua sare kisipuuzwe."*

***Maoni ya Mtangazaji**: "nakumbuka Novemba 2016, Rais Dk. John Magufuli alifanya ziara ya kushtukiza katika gereza la Ukonga jijini Dar es salaam. Akiwa gerezani hapo alisema kuwa madhumuni ya ziara hiyo ilikuwa ni kuzungumza na askari baada ya kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambapo alimsindikiza Rais wa Zambia. Nafikiri hata kule alipokuwa*

*Butimba kuna kamanda mmoja alisema unaona hizi sare tunapendeza hivi tunajinunulia wenyewe kwa sababu kazi tunaipenda...".*

*"Mama asimulia machungu ya mume ni habari inapatikana ukurasa wa 5, mlalamikaji, Aurelia Sirili amedai kutelekezwa katika nyumba ya kupanga baada ya mumewe na wakwe zake kuhamia katika nyumba aliyojenga kwa mkopo wake... Aurelia (31) umri wake huo ambaye ni mwalimu katika shule ya sekondari Ituha jijini Mbeya ameiomba Mahakama ivunje ndoa yake na mumewe, Mode Mbwiga kutokana na kitendo hicho alichomfanyia".*

*"Majaliwa aagiza kutiwa mbaroni kwa wezi wa tani tano za nondo... Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa, ameagiza Kamanda wa Polisi mkoa wa Kilimanjaro, Hamisi Issa, awasake na kuwatia mbaroni watu waliohusika na wizi wa tani tano za nondo...".*

*"Malima aongoza mazishi ya mwandishi wa UPL, Mkuu wa mkoa wa Mara, Adam Malima ameongoza baadhi ya wakazi wa mkoa wa Mara kumzika aliyekuwa mwandishi wa habari wa kampuni ya Uhuru Publications Limited (UPL) inayochapisha magazeti ya Uhuru, Mzalendo na Uhuru Weekend, Eva Sweet Musiba (44) mkoani humo... Eva Sweet alifariki dunia Julai 17 mwaka huu wakati akipatiwa matibabu katika hospitali ya Musoma mkoani Mara...".*

***Habari Leo:** "Majaliwa akerwa na hujuma kituo cha mabasi Moshi, Wazari Mkuu, Kassimu Majaliwa amesikitishwa na hujuma dhidi ya kituo kikuu cha mabasi, Nganga Mfumuni mjini Moshi utakachogharimu zaidi ya Sh. bilioni 9 na kutishia kusitisha fedha za kumalizia mradi huo kama kuna ubadhilifu...".*

*" Kuna habari picha hapa ikimuonesha Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania namuona hapa na hawa wahudumu wa ndege lakini pia kuna kamanda hapa anashuka ngoja ntakueleza maelezo yake, Rais John Magufuli akisalimiana na wahudumu wa ndege iliyomchukua baada ya kuteremka katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage jijini Dar es salaama akitokea Dodoma jana, picha na Ikulu picha nzuri kabisa na mwana dada huyu anapiga goti wakati huo anasalimiana na Rais halafu mwandishi ameinasa palepale...".*

## 2.0 WITO WA KUFIKA MBELE YA KAMATI YA MAUDHUI

Tarehe 23 Agosti, 2019 Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa TBC FM Radio wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi kwa nini wasichukuliwe hatua. Wito huo pia uliutaka uongozi huo ulete utetezi wa kimaandishi.

Tarehe 27 Agosti, 2019, saa 08:00 mchana, uongozi wa Kituo cha TBC FM Radio ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini kituo hicho kisichukuliwe hatua kutokana na

tuhuma za kukiuka agizo la Serikali linalowataka watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma kwa undani maudhui yaliyopo katika magazeti na badala yake wasome vichwa vya habari pekee. Katika kutoa utetezi wake, TBC FM Radio iliwakilishwa na Aisha Dachi, Mkurugenzi wa Redio, Alex Magwiza, Meneja wa Redio, na Athuman Iddy, Mkuu wa TBC FM.

## 3.0 KUSIKILIZA KIPINDI CHA BUSATI CHA TAREHE 02 AGOSTI, 2019

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa TBC FM Radio walisikiliza kipindi cha Busati cha tarehe 02 Agosti, 2019 kilichorushwa na TBC FM Radio ili kujiridhisha iwapo kituo hicho kilikiuka agizo tajwa la Serikali.

## 4.0 MAELEZO YA UTETEZI YA TBC FM RADIO

Uongozi wa TBC FM Radio uliwasilisha utetezi wao wa maandishi kwa Kamati.

Katika utetezi wao huo, TBC FM Radio wameomba radhi kwa kosa walilolifanya na kwa usumbufu wo wote uliojitokeza. Wameeleza kuwa kosa hilo lilifanyika kwa sababu kipindi kiliendeshwa na mtangazaji mbadala aliyekuwa hana uzoefu na kipindi hicho baada ya mtangazaji anayehusika kuugua ghafla. Hata hivyo, wameeleza na kutambua kuwa kipindi kuendeshwa na mtangazaji asiye na uzoefu haikuwa sababu ya msingi kwa sababu mtangazaji anatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni, katazo/maelekezo ya Serikali na weledi. Walimalizia kwa kusema kuwa walishamchukulia hatua stahiki mtangazaji kwa kumuandikia barua ya kumtaka ajieleze kimaandishi na kisha kumpatia onyo la mdomo. Walikabidhi barua hizo kwa Kamati.

TBC FM Radio iliendelea kutoa maelezo ya utetezi wa mdomo kama ifuatavyo;

4.1 **Aisha Dachi** ambaye ni Mkurugenzi wa TBC FM Radio alianza kwa kukiri kosa na kuomba radhi. Alisema kuwa walishaligundua kosa hilo na tayari wameshawachukulia hatua za kinidhamu Msimamizi wa Kipindi, Salome Baptister na Mtangazaji, Mbazigwa Hassan. Kwamba msimamizi alitakiwa kujieleza kimaandishi na kisha kupewa onyo la mdomo kwa sababu ni kosa lake la kwanza. Mtangazaji alipewa onyo la mdomo. Alimalizia kwa kusema kuwa wanatambuwa kuwa TBC FM Radio ni chombo cha umma na wanapaswa kuwa mfano kwa vyombo vingine kwa kufuata Sheria, Kanuni na maelekezo ya Serikali pamoja na kuzingatia weledi na maadili ya uandishi wa habari.

4.2 **Alex Magwiza** ambaye ni Meneja wa Redio alisema kuwa pamoja na kuwachukulia hatua stahiki wahusika walifanya uzembe huo, pia kwenye vikao vyao vya kiofisi vya kila juma wamekuwa wakiwasisitiza wafanyakazi wote kuhusu kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo yote ya Serikali.

## 5.0 MAJUMUISHO YA UTETEZI

Katika kujumuisha utetezi wao, **Aisha Dachi** aliendelea kuomba radhi kwa kosa lililotokea.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba kituo cha TBC FM Radio kupitia kipindi chake cha Busati, kipengele cha Magazeti kimekiuka agizo la Serikali la kutosoma habari za magazetini kwa undani;

6.2 Hata hivyo, Kamati ya Maudhui imeridhishwa na hatua walizochukua Uongozi wa TBC FM Radio za kuwataka Msimamizi wa Kipindi na Mtangazaji waliotenda kosa kujieleza na kisha kuwapa onyo;

6.3 Kamati pia imezingatia kitendo cha Uongozi wa TBC FM Radio kuwasilisha vielelezo vya hatua za kinidhamu walizowachukulia wahusika;

6.4 Pia, Kamati imetilia maanani ushirikiano ulioonyeshwa na Uongozi wa TBC FM Radio ikiwa ni pamoja na kukiri kosa lao na kuomba radhi.

## 7.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA TBC FM RADIO

Kamati ina lengo la kuimarisha fani ya utangazaji na kamwe haina nia ya kubana au kuzuia ubunifu wa watangazaji, bali inawataka watangazaji kuboresha kazi zao kwa kuandaa na kutangaza maudhui yanayozingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya fani ya uandishi na utangazaji wa habari nchini.

Kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa TBC FM Radio mambo yafuatayo;

7.1 TBC FM Radio ni chombo cha umma na hivyo kinapaswa kuwa mfano mzuri kwa vyombo vingine pamoja na kuongoza njia kwa kuhakikisha kinazingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Maelekezo, Miongozo Na Makatazo ya Serikali, pamoja na weledi na maadili ya taaluma ya uandishi wa habari;

7.2 Kuimarisha na kuboresha usimamizi, utayarishaji na utangazaji wa vipindi vyao.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kusikiliza maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi TBC FM Radio, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa kituo cha TBC FM Radio kupitia kipindi chake cha **Busati** kimekiuka agizo la Serikali

kutosoma habari za magazetini kwa undani kama ilivyoelezwa katika tathmini hapo juu.

Hivyo, Kamati ya Maudhui inaamua kukipa **Onyo** kituo cha TBC FM Radio na kukiagiza kutorudia kosa kama lililojitokeza katika shauri hili.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam siku hii ya tarehe **03** mwezi **Septemba**, mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bi Valerie Ndeinengo-Sia Msoka**

.....................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Joseph Method Mapunda** .......................................
2. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**.......................................
3. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**.......................................
4. **Bwana Jacob Gregory Tesha**.......................................